JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TANGAZO
KWA WANANCHI WOTE

MREJESHO WA UANDAAJI WA MPANGO NA BAJETI YA HALMSHAURI YA MJI WA TARIME KWA MWAKA 2018/2019

Imeandaliwa na:-
Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji Tarime
S.L.P. 45
TARIME

October, 2018

MREJESHO WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/2019

1.0. UTANGULIZI

Mh. Mwenyekiti,

Kama ilivyo ada kila mwaka Halmashauri ya Mji huandaa Mpango na Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa mwaka unaofuata kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa Mpango na Bajeti pamoja na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Mpango huu uliwasilishwa katika vikao vya kisheria vya Halmashauri ya Mji na kuidhinishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Tarime kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango na Kamati ya Bunge la Serikali za Mitaa kwa ajili ya uchambuzi.

2.0. BAJETI ILIYOIDHINISHWA

Mhe. Mwenyekiti,

Napenda kuijulisha Baraza lako kwamba kazi hiyo ilikamilika vizuri na tayari Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 na imeanza kutumika.

Kulingana na ukomo wa bajeti **(Budget Ceiling)** iliyotolewa na Wizara ya Fedha kwa mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Mji wa Tarime imeidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi 18,966,120,000.00** kwa ajili ya shughuli za matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo.

Kati ya fedha hizo **shilingi 1,220,637,000** kutokana na vyanzo vya ndani, **Shilingi 631,241,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), **shilingi 14,143,456,000** kwa ajili ya mishahara (PE), **shilingi 2,378,001,000** ruzuku ya maendeleo kutoka Serikali kuu (Fedha za ndani) na **shilingi 592,785,000** kutoka kwa Wahisani mbalimbali. Aidha jumla ya **Tsh. 1,116,407,836** zilivuka mwaka yaani bakaa.

3.0. BAJETI YA NYONGEZA (SUPLIMENTARY BUDGET)

Mhe. Mwenyekiti,

Baada ya maandalizi ya bajeti ya kawaida kulingana na ukomo wa bajeti uliopitishwa na Wizara ya Fedha, Halmashuri ya Mji imetengewa jumla ya **Tsh. 1,079,432,740** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia Wahisani na Wadau wengine wa maendeleo. Kati ya fedha hizo **Tsh. 400,000,000** kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya **(CDG)**, **Tsh. 368,925,000** kutoka Equip Tanzania, **Tsh 110,000,000** kutoka Mamlaka ya

Elimu Tanzania **(TEA), Tsh 48,000,000** kutoka **AGPAH, Tsh. 9,622,740** Mnara - Turwa S/Msingi na **Tsh. 142,885,000** kutokana na michango ya wananchi (Tarime na Mogabiri Sec).

4.0. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

Mh. Mwenyekiti,

Bajeti ya Halmashauri ya Mji Tarime imepungua kwa **18%** baada ya ukomo wa bajeti kutolewa na Wizara ya Fedha ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2017/2018. Upungufu huo unatokana sababu zifuatazo:-

i. Baadhi ya vyanzo vikuu vya ndani vya Halmashauri kama vile kodi ya majengo, ushuru wa mabango na kodi ya ardhi kuondolewa kwenye orodha ya vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
ii. Mishara (PE) imepungua kutokana na watumishi waliondolewa kwenye orodha ya malipo baada ya matokeo ya uhakiki wa vieti feki
iii. Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) kutopata kabisa mgao **(Ceiling)**
iv. Miradi ya Maendeleo ya kupitia Wahisani (SEDP) kutopata kabisa mgao **(Ceiling)**
v. Kupungua kwa ukomo wa bajeti ya ruzuku ya uendeshaji (OC) na miradi ya maendeleo kupitia Wahisani mbalimbali (HSBF na NWSSP).

Hali hii imepelekea miradi mingi iliyokuwa imepangwa kupitia fedha za LGDG, SEDP, HSBF, NWSSP kuathirika na kuondolewa kwenye mpango. Hii ni kutokana na fedha za ndani pekee kutotosheleza utekelezaji wa miradi yote iliyokuwa imelengwa.

5.0. MPANGO ULIOPO

Mh. Mwenyekiti,

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ilifungua dirisha la andiko Miradi kwa ili kuwajengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato kwa lengo la kuwawezesha kujitegemea wenyewe badala ya kutegemea ruzuku toka Serikali Kuu.
Kutokana na fursa hiyo Halmashauri ya Mji Tarime imeandaa maandiko ya miradi ikijumuisha Mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Tarime Mjini na Mradi wa ujenzi wa stendi mpya Kemange.

i. Mradi wa Soko linatarajiwa kuwa na jumla ya maduka 406, Vizimba 196, Migahawa 2, Mabenki 2, maeneo 4 ya wazi ya soko na bucha 6. Mradi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya **Tsh. 8,073,148,416** hadi kukamilika na unatarajia kukusanya jumla ya **Tsh. 671,040,000** kwa mwaka.

ii. Mradi wa Stendi unatarajiwa kuwa na maduka 279, choo cha abiria 1, Stoo 1, Migahawa 4, Ofisi 1, Kituo cha Polisi, na chumba cha kupunzikia abiria. Stendi hii mpya inakadiriwa kuhudumia magari 80 kwa siku na inakadiriwa kugharimu jumla ya **Tsh. 4,000,511,374.80** hadi kukamilika. Mradi ukikamilika unakadiriwa kuingiza jumla ya **Tsh. 245,280,000.**

Mh. Mwenyekiti,

Kutokana na vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Fedha na Mipango vya kufuzu kupata fedha za mradi, mpaka sasa kwa upande wa Halmashauri ya Mji Tarime mradi yote miwili imeandaliwa, kuwasilishwa na imepokelewa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

Naomba kuwasilisha,

Pedas K. Maungwa
KAIMU MKURUGENZI WA MJI
HALMSHAURI YA MJI
TARIME

MCHANGANUO WA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI
BAADA YA UKOMO WA BAJETI, BAKAA NA BAJETI YA NYONGEZA (SUPLIMENTARY)

Na.	Aina ya Chanzo	Makisio ya Mapato 2018/2019	Makisio ya Matumizi 2018/2019
1	Vyanzo vya ndani (Own source)	1,220,637,000	1,220,637,000
2	Ruzuku ya kufidia vyanzo vilivyofutwa (GPG)	49,415,000	49,415,000
3	Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC)	581,826,000	581,826,000
4	Ruzuku ya Mishahara (PE)	14,143,456,000	14,143,456,000
5	Constituency Development Catalist Fund (CDCF)	33,767,000	33,767,000
6	Primary Free Education Programme	300,954,000	300,954,000
7	Secondary Free Education Programme	543,280,000	543,280,000
8	Rural Water Suply and Sanitation Programme (RWSSP)	104,973,000	104,973,000
9	Health Sector Bascket Fund (HSBF)	158,912,000	158,912,000
10	Maji Vijijini (Ujenzi wa vyoo)	328,900,000	328,900,000
11	Hospitali za Wilaya	1,500,000,000	1,500,000,000
	Jumla	**18,966,120,000**	**18,966,120,000**
	Bakaa toka 2017/2018		
1	Miradi ya Maendeleo (CDG)	477,087,257	477,087,257
2	Makato ya Mishahara kisheria	6,745,505.27	6,745,505.27
3	Miradi ya Maji (NWSSP)	53,830.04	53,830.04
4	Equip - Tanzania	220,285,514.59	220,285,514.59
5	Buscket Fund	5,133,465.74	5,133,465.74
6	Global Fund	8,034,741.34	8,034,741.34
7	UNICEF	29,442,400	29,442,400
8	Elimu Bila Malipo	52,079,153.3	52,079,153.3
9	Mapato ya ndani (Ownsource)	56,511.77	56,511.77
10	Matumizi Mengineyo (OC)	418,404,977	418,404,977
11	Ada pamoja na Michango ya wananchi shuleni	3,429,303.16	3,429,303.16
	Jumla	**1,220,752,659**	**1,220,752,659**
	Bajeti ya Nyongeza (Supplementary)		
1	Ujenzi wa Kituo cha Afya (CDG)	400,000,000	400,000,000
2	Equip Tanzania	368,925,000	368,925,000
3	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)	110,000,000	110,000,000
4	AGPAHI	48,000,000	48,000,000
5	Mnara wa Voda (Turwa S/M)	9,622,740	9,622,740
6	Michango ya Wananchi shuleni	142,885,000	142,885,000
	Jumla	**1,079,432,740**	**1,079,432,740**
	JUMLA KUU	**21,266,305,399**	**21,266,305,399**